JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA ARUSHA

MTIHANI WA KIDATO CHA PILI

HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI

MWONGOZO WA USAHIHISHAJI

SEHEMU A (ALAMA 15)

1. ALAMA 10@1.

SWALI	I	II	III	IV	V	VI	VII	VIII	IX	X
JIBU	D	B	A	B	B	C	B	C	D	C

2. ALAMA 05@1

ORODHA 'A'	I	II	III	IV	V
ORODHA 'B'	B	A	C	D	F

SEHEMU B (ALAMA 70)

3. i) Kutambulisha utu wetu

ii) Kukuza na kuendeleza Ulusiano wa kariba miongoni mwa watu katika jamii

iii) Kujenga heshima na kuminiana miongoni mwa watu katika jamii

iv) Upatikanaji wa haki, usalama, usawa na furaha katika jamii

v) Kutunza na kuhifadhi historia ya Taifa.

Alama 10@2

i) Mafunzo ya elimu ya jinsia
ii) Mafunzo ya kujenga umoja na mshikamano
iii) Mafunzo ya maadili ya jamii
iv) Mafunzo ya ujuzi wa kazi mbalimbali za kijamii.
v) Mafunzo ya lugha za kijamii
vi) Mafunzo kwa ajili ya kulinda, kusimamia rasilimali zao na kutatua migogoro baina yao.

Hoja tano (5) Alama 10 @2.

5. i/ Maeneo ya kuwekeza mitaji yao ya kibiashara ili kupata faida kubwa.
ii) Mahitaji ya masoko mapya ya bidhaa zilizozalishwa na viwanda vyao
iii/ Mahitaji ya matighafi kwa ajili ya viwanda Mfano; kilimo cha mazao ya biashara na madini.
iv) Matamanio yao makubwa ya kueneza dini ya kikristo katika maeneo mbalimbali kupitia wamisionari wa mwanzo hasa barani Afrika.
v/ Ushindani wa kisiasa na kijeshi kwa mataifa ya ulaya magharibi katika kutawala maeneo makubwa. Mfano Sehemu muhimu za kimkakati kwa njia za bahari ya Atlantiki na Mediterania kupita bahari ya shamu hadi bahari ya hindi.
vi/ Mahitaji ya maeneo ya kuanzisha makazi ya watu wasio na shughuli maalumu huko ulaya.
Hoja tano, Alama 10 @2.

i/ Kutoweka kwa umoja na mshikamano katika jamii za kitanzania.

ii/ Kufa/Kutoweka kwa utamaduni wa kijadi.

iii/ Kupungua kwa matumizi ya lugha za asili na kuimarisha lugha za kigeni. Mfano lugha ya kiingereza kuwa lugha rasmi.

iv/ Kufa/kudhofu kwa elimu ya jadi na kuanzishwa kwa elimu na maadili ya kigeni.

v/ Kudumaa kwa tiba za asili na kuanzishwa kwa mitindo na mfumo mpya wa tiba za kigeni mfano tiba za ulaya:

Alama 10 @2.

7. i/ Ukuaji wa lugha ya kiswahili katika mawasiliano baina ya jamii za kitanzania na zile za mashariki ya mbali na kati.

ii/ Kuenea kwa dini ya kiislamu

iii/ Kuenea kwa utamaduni wa kigeni
mf. Mila na desturi; vyakula, mavazi n.k

iv/ Kukua kwa miji ya pwani. Mfano, Bagamoyo, Kilwa, Zanzibar n.k

Hoja 5; 10@2

v/ Kukua kwa utawala wa kiaraby

vi/ Ujenzi wa nyumba za mitindo ya kigeni. Mfano Mitindo ya kiaraby n.k.

v/ Kukua na kuenea kwa biashara ya utumwa.

i/ Mahitaji ya jamii: Uvumbuzi na uboreshaji wa mashq ya jamii za kitanzanwa.
Mfano. mbinu za kilimo.

ii/ Elimu ya jadi kuhusiana na mazingira, historia na utamaduni wa jamii husika.

iii/ Mazingira ya kijiografia, Mfano maendeleo ya teknolojia ya asili kwa usafiri, uvuvi na uhifadhi wa chakula.

iv/ Uhamaji: kueneza maarifa na ujuzi katika maeneo mbalimbali.

v/ Rasilimali za asili kama vile madini, mbao n.k.

vi/ Biashara na ushirikiano katika kubadilishana mazao, teknolojia na utamaduni.

Hoja 5 Alama 10 @ 2.

9. i/ Mabadiliko ya hali ya hewa na mazingira.
Jamii zilihama kutoka eneo moja kwenda jingine ili kutafuta mazingira bora ya mashq. Mfano; maji, malisho ya wanyama, Ardhi yenye rutuba n.k.

ii/ Migogoro ya Ardhi. Migogoro mifano ya kugombania mipaka, mashamba n.k ilipelekea jamii kuhama.

iii/ Sababu za uhusiano wa kijamii, ndoa na familia (kuoa na kuolewa)

iv/ Mipasuko katika koo zao

v/ Majanga kama vile vita, magonjwa, ukame n.k

SEHEMU C (ALAMA 15)

UTANGULIZI

Mwanafunzi aeleze kwa ufupi tafsiri ya neno maadili au mmomonyoko wa maadili katika jamii (angalau Mistari 3-4, Alama 1½)

KIINI

Mwanafunzi aorodheshe na kufafanua kwa kina hoja tano kama mikakati anayopendekeza katika kukuza na kudumisha maadili katika jamii za kitanzania. Mfano hoja zifuatazo;

i) Kupandisha elimu ya maadili kuanzia ngazi ya familia.

ii) Kujumuisha mafunzo ya maadili katika mitaala ya elimu. Mf. kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu.

iii) Kuhimiza mafundisho mazuri ya dini na imani kama msingi ya maadili katika jamii

iv) Kuhamasisha maadili kupitia vyombo vya habari na mitandao katika jamii. Mfano redio, luninga, magazeti n.k.

v) Kuzingatia kuwa na uongozi bora na utawala wa kisheria. Sheria zizingatiwe na kusimamiwa bila upendeleo.

vi) Kukuza utamaduni wa asili wa kitanzania kwa kuwashirikisha wazee na viongozi wa jadi katika malezi ya vijana

vii) Kujenga mazingira wezeshi ya kiuchumi kwa jamii na taifa kwa ujumla

HITIMISHO

Mwanafunzi atoe maoni/Mapendekezo/ Ushauri n.k. Mfano chanzo cha mmomo nyoko wa maadili katika jamii.

Alama 1.5.